

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**



**ORODHA YA SHUGHULIZA LEO**

**MKUTANO WA ISHIRINI**

**KIKAO CHA AROBAINI NA TANO**

**06 JULAI, 2015**



# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA ISHIRINI

KIKAO CHA AROBAINI NA TANO – TAREHE 06 JULAI, 2015

I. TAARIFA YA SPIKA:

II. MASWALI:

OFISI YA WAZIRI MKUU:

**312. MHESHIMIWA ASSUMPTER NSHUNJU  
MSHAMA (NKENGE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-  
Wilaya ya Misenyi ni miongoni mwa Wilaya  
mpya na inakabiliwa na tatizo kubwa la maji  
kwa mji wote wa Bunazi:-

(a) Je, kwa nini Serikali haijapeleka maji  
katika mji huo;

(b) Mto Kagera umezunguka Wilaya ya  
Misenyi; Je, ni lini Serikali itaupatia maji  
ya bomba mji huo kutoka mto huo.

**313. MHESHIMIWA SAID AMOUR ARFI  
(MPANDA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-

Je, Serikali ina mpango gani wa muda mfupi na mrefu wa kutatua tatizo la uhaba wa vyumba vya madarasa kwa shule za msingi na sekondari nchini pamoja na madawati badala ya kutegemea nguvu za Wananchi.

**WIZARA YA KAZI NA AJIRA:**

**314. MHESHIMIWA HAMOUD ABUU JUMAA  
(KIBAHA VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kazi na Ajira:- Kuna vijana wengi katika Jimbo la Kibaha Vijijini ambao wamejiajiri wenyewe:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwawezesha vijana hao kwa kuwakopesha fedha na kuwapa elimu ya ujasiriamali ili waweze kujikwamua kiuchumi.

## **WIZARA YA UJENZI:**

### **315. MHESHIMIWA FELISTER ALOYCE BURA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:- Serikali iliamua kujenga kwa lami barabara ya kutoka katika mzunguko wa Shabiby hadi Chako ni Chako kwa nia ya kupunguza msongamano wa magari makubwa kuingia mjini:-

Je, ni lini barabara hiyo itajengwa.

### **316. MHESHIMIWA KURUTHUM JUMANNE MCHUCHULI (VITI MAALUM):**

- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, ni lini Serikali itafungua barabara ya Kisasi (Morogoro) hadi Mloka Rufiji.

## **WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:**

### **317. MHESHIMIWA NYAMBARI CHACHA NYANGWINE (TARIME):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:- Tanzania ni nchi ya pili duniani kwa kuwa na vivutio vingi vya Utalii ikitanguliwa na Brazil lakini ni miongoni mwa Nchi zinazopokea Watalii wachache sana:-



- (a) Je, ni sababu zipi za msingi zinazosababisha kutokea kwa hali hii;
- (b) Je, Serikali ina mkakati gani endelevu wa kutangaza Sekta ya Utalii ili kuwafanya watalii wengi kuja kutembelea vivutio hivyo;
- (c) Je, kwa nini Serikali kwa kushirikisha taasisi zake za TTB, TANAPA, NGORONGORO nk isianzishe Utalii wa kiutamaduni (Cultural Tourism) ili kuongeza vivutio vya Utalii hapa nchini.

**WIZARA YA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:**

**318. MHESHIMIWA KHATIB SAID HAJI (KONDE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:- Kwa muda mrefu kumekuwa na ushiriki usioridhisha kwa timu zetu za mpira wa miguu na ndondi katika mashindano ya kimataifa:-

Je, Serikali inachukua hatua gani ili kuliondolea taifa hili aibu ya kushindwa mara kwa mara katika mashindano ya kimataifa.

## **WIZARA YA MAJI:**

### **319. MHESHIMIWA AMINA NASSORO MAKILAGI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:- Ilani ya CCM ya Mwaka 2010 – 2015 (IX) limetamka wazi kuwa Serikali itatunga Sheria itakayowataka wote wanaojenga nyumba bora Mjini na Vijijini kuweka Miundombinu ya kuvuna Maji ya Mvua:-

- Je, Serikali imefikia hatua gani katika utekelezaji wa dhamira ya Serikali ya kuhakikisha wananchi wanaondokana na tatizo la ukosefu wa Maji.

## **WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:**

### **320. MHESHIMIWA KAPT. JOHN ZEFANIA CHILIGATI (MANYONI MASHARIKI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi:- Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ina utaratibu wa kuruhusu uanzishaji wa sekondari za Kidato cha Tano na Sita; na Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni ilishapendekeza Shule za Sekondari za Chikuyu na Kizigo zianzishwe Kidato cha Tano na Sita (“A” level):-

Je, ni lini Wizara hii itatoa kibali kwa shule hizo mbili kuanzishwa kidato cha tano na sita hasa ikizingatiwa kuwa zimekidhi vigezo vya idadi ya Walimu, Maabara na hosteli.

### **III. MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI:**

**(Kusomwa Mara ya Pili, Kamati ya Bunge zima na kusomwa Mara ya Tatu)**

Muswada wa Sheria ya Usimamizi wa Mapato ya Mafuta na Gesi wa Mwaka 2015 (*The Oil and Gas Revenue Management Bill, 2015*).

Muswada wa Sheria ya Uwazi na Uwajibikaji katika Tasnia ya Uchimbaji Tanzania wa Mwaka 2015 [*The Tanzania Extractive Industry (Transparency and Accountability) Bill, 2015*].

**(Majadiliano yanaendelea)**

**DODOMA  
06 JULAI, 2015**

**DKT. T. D. KASHILILAH  
KATIBU WA BUNGE**